Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 80 No. 217 | DH.QAD-DH.HIJ.1440AH | AGOSTI 2020 | ZAHOOR 1399 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

Na bila shaka Tumewaelezeawatu namna kwa namna katika Qur'an hii kila mfano; lakini mwanadamu amezidi kila kitu kwa ubishi. (Al Kahf 18:55)

## Baada ya COVID-19: Uchumi wa Islam ndio Muarobaini?



*Makala uk 2*

## Uongozi Katika Islam

Na **Mwandishi Wetu**



Islamu imetoa Uongozi baina ya Mwanaume na Mwanamke kwa sababu kadhaa. Uongozi kwa sababu mbalimbali kama;

1 Majukumu yake,

2 Tofauti ya Uumbaji wake.

Mwanaume amepewa majukumu mengi juu ya Mwanamke kiasi hiki Mtume s.a.w alisema, Mwanaume hakuna anachodai kwa mke wake ila Unyumba tu. Na majukumu haya yapo ili kumrahisishia Mwanamke naye atakeleze wajibu

*Endelea uk. 5*

## Maarifa Juu ya Jahanamu na Pepo

Na **Musa Mgeleka**
**Dar es salaam**



*Makala uk 4*

Uchaguzi au Uteuzi!? uk. 2

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

## Uchaguzi au Uteuzi

Hapana shaka umewahi kukutana na dhana hii ya *Taasisi ya kuchagua* na kusikia maneno *Huzur alichaguliwa* Khalifatul Masih katika msamiati wa Jamaat. Tunadhani pana haja ya kufafanua dhana hii ya kuchagua.

Kila Ahmadiyya wakiwemo na watoto wanajua fika kuwa ni Allah pekee Anayemuinua mja na kumpa cheo cha Khalifa. Hili tunajifunza kutoka Qur'an Tukufu ambamo Allah Mwenye uwezo anaeleza bayana: "Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi... (24:56)

Akifafanua aya hii kutoka Sura Al-Nur, Khalifatul Masih wa II r.a. anasema; Wale wanaosema watu walimchagua Khalifa wanatakiwa waone aibu na wasije kukataa amri za Allah Mwenye uwezo. Binadamu alivyo dhaifu na asiyejiweza atatoa wapi nguvu na uwezo wa kupandisha daraja la mwingine. "*Innal Fadhila Bi Yadillah*" (Fadhila zote zimo mkononi mwa Allah). Ni uchaguzi wa Allah pekee unaompandisha hadhi mtu yeyote na si vinginevyo. Binadamu ana elimu haba na mpungufu wa kuchambua mambo. Ni kazi ya Mwenye ujuzi wa kila kitu kumtwisha mzigo anayefahamu anafaa. (*Khilafat Ala Minhajin-Nabuwaah, Juzuu 1*)

Ukweli wa mambo ni kwamba Allah Anapomteua Nabii hakuna kuongea au kupunguza neno ni kutii tu. Watu wanaanza kukusanyika na kundi la waaaminio linapatikana (Jamati). Anapofariki Nabii, Allah Anaibariki Jamati hiyo ya Nabii kwa kuipatia fursa kuamsha mikono yao kwa yule ambaye Allah tayari Amemchagua naye ndiye Khalifa.

Historia ya taasisi ya kuichagua inaanzia toka enzi za Hadhrat Umar r.a. Khalifa wa pili wa Nabii wa Islam. Akiwa kitandani anaumwa aliteua kamati ya watu sita ili wachague Khalifa akisha kufa. Makhalifa wote walioongoka wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. walichaguliwa kwa "***Shura***" (kushauriana) pamoja na wazee wa Jamati.

Utamaduni huo umeendelezwa katika Khilafat-e-Ahmadiyya lakini pasiwe na shaka yoyote kama ilivyoeleza hapo juu kuwa hakuna binadamu au taasisi inayoteua Khalifa. Uchaguzi unaofanyika ni kielelezo tu cha matakwa ya Allah.

***Lakini ushahidi gani tulio nao kuwa Khalifa anachaguliwa na Allah***? Huduma yake, dhamira yake, kukubaliwa kwa maombi yake na kustawi, mafanikio na maendeleo ya Jamati ni ushahidi ulio wazi wa kuteuliwa na Allah.

Historia inatoa ushahidi kuwa chini ya Khilafat-e-Ahmadiyya Jamaat Ahmadiyya imepata mafanikio na maendeleo licha ya mashaka na viunzi vingi vilivyoletwa na watu binafsi. Serikali na taasisi. Makundi yote yaliangamia na kusambaratika wakati Jamati Ahmadiyya chini ya Khilafat-e-Ahmadiyya inazidi kupanda juu ya vilele vya mafanikio.

# Athari za COVID-19: Uchumi wa Kiislam ndio Muarobaini?

Imefasiriwa na
Mahmood Hamsin Mubiru

Taarifa kuhusu janga la Covid-19 zimepokelewa kutoka kila pembe, na kila pembe ikitoa takwimuu kuhusu vifo, wangapi wamepoteza kazi, walioathirika kisaikolojia, waliopata faidika, kufa kufaana.

Kwa ufupi tafiti zote hizo na taarifa zote zimetoa ujumbe mzito kuwa uchumi wa dunia umo katika chumba cha wagonjwa mahututi. Viongozi wa dunia bila shaka kila wanachoshika kinadondoka kwa hofu ya kilicho mbele yao.

Kwa wale viongozi waliofunga mipaka yao, na wale walioendelea kufungua hali ya matibabu ilivyoendelea kudorora lawama zote walibebeshwa viongozi.

Kila nchi imeathirika kwa njia moja au nyingine lakini kwa ujumla zote zimeathirika kiuchumi.

Ikiwa nchi zote ziko ukingoni mwa shimo la maangamizi, swali tutaepuka vipi kutumbukia katika shimo hili? Wakati nchi nyingine zimeanza kufufua viwanda vyao wengine wanadhani hiyo haitakuwa nia pekee ya kuwaokoa.

Mataifa yenye bahati ni yale ambayo yana washauri wa uchumi ambao wanawaambia kwamba ubepari hauwezi tena kufanya kazi kwa sasa. Nchi za Magharibi zinaitizama Uchina na kuona mfano mzuri wa kuiga. Uchina kwa upande wake imeumia sana chini ya ukomunisti na imechukua mengi kutoka kwenye ubepari. Serikali itatawala uchumi wakati huo huo ikiruhusu mtiririko wa soko huria na huo ni mchanganyiko wa ujamaa na ubepari.

Wanauchumi wa Magharibi wanapenda kuita mfumo huo wa China – 'njia ya tatu'. Hata hivyo njia hii ya tatu bado haijaelezwa vizuri, mfumo wa China hauwezi kuitwa njia ya tatu kutokana na athari za ubepari wakati pazia ya ujamaa iko pale kufunika kile kinachoendelea.

'Njia ya tatu' bado hawajaitambua na uchumi wa dunia, nia hiyo kwa hakika ni Uchumi wa Islam. Jumuiya ya Ahmadiyya kwa miongo sasa imekuwa ikihubiri mfumo huo lakini watu wengi wameendelea kupuuza mahubiri hayo.

Wakati sasa ni dhahiri kwamba dunia haiwezi tena kurudi kwenye ubepari ni wakati mzuri wa kuieleza dunia tulichokuwa tunahubiri miaka yote hiyo.

Hadhrat Mirza Bashirudin Mahmood Ahmad, Khalifatul Masih II wa Jumuiya ya Ahmadiyya amefafanua bayana kabisa jinsi Islam inavyoruhusu soko huria chini ya usimamizi wa Serikali na hii ndio jibu pekee kuhusu kushindwa kwa ubepari na ujamaa. Mfano wa Kiislam ni hotuba aliyoitoa Khalifatul Masih wa II mwaka 1945 mahali ambapo kuna soko huria wakati Serikali inachunga usalama wa nchi. Hii ndio njia pekee ya kuleta mafanikio. Riba lazima iwekwe pembeni na zitafutwe njia nyingine za kukopa na wakati kutokomeza unyonyaji wa wale walio dhaifu katika jamii.

Ni katika mfumo wa Islam tu ambamo wenye uwezo wanatoa mali kwa ajili ya wanyonge kwa njia ya Zakat.

Tukija kwenye mfumo unaotekelezwa na Jumuiya ya Ahmadiyya upo utaratibu wa Wassiyyat – ambao asilimia 10 ya mali zako zinatolewa kwa ajili ya manufaa ya jamii – na huo ndio mfano wa kipekee ambapo mali inaendelea kuwa mikononi kwa mtu binafsi lakini bado mali ile inatoa mchangp kwa manufaa ya jamii kwa ujumla. Maelezo ya kina kuhusu utaratibu huu unapatikana katika kazi nyingine maarufu ya Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad r.a. Nizam-e-Nau – Mfumo Mpya wa Dunia.

Wakati wa Mkutano wa nchi zenye uchumi wenye nguvu duniani – G20, Waziri wa Fedha wa Ujerumani Wolfgang Schaeuble aliweka bayana kuwa – mtizamo wa islam kuhusu uchumi wa dunia ni muhimu na dunia inatakiwa iutizame kwa jicho la pili.




*Waziri wa Fedha wa Ujerumani Wolfgang Schaeuble, kushoto, akiongea katika moja ya mikutano ya G20*

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

# Muongozo kwa Makatibu wa Waqfiin-e-Nau

Na: **Latif Mosse**



*Khalifa Mtukufu wa V^atba akihutubia Kozi kwa Makatibu wa Waqf-e-Nau Duniani mwaka 2019*

Bismillah Rahman Rahim

**Muongozo muhimu kwa ajili ya makatibu wa Tahrik Waqf-e-nau**

اِذْ قَالَتِ امْرَاَتُ عِمْرٰنَ رَبِّ اِنِّیْ نَذَرْتُ لَکَ مَا فِیْ بَطْنِیْ مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّیْ ۚ اِنَّکَ اَنْتَ السَّمِیْعُ الْعَلِیْمُ

*(Kumbukeni) aliposema mwanamke wa Imrani: Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye.* (3:36)

Pindi mwanamke wa Imran alipoahidi kwa mola wake juu ya kitakachozaliwa baadae, alitoa pia kauli hii kuwa sikuahidi tu kilichomo tumboni kwangu kama ibada tu ya zamani ila kwa sababu kubwa ambayo ni;

وَ اِنِّیْۤ اُعِیْذُہَا بِکَ وَ ذُرِّیَّتَہَا مِنَ الشَّیْطٰنِ الرَّجِیْمِ

*nami hakika namkinga Kwako, yeye na wazao wake, Uwalinde na shetani arujumiwaye.*(3:37)

Kama tunavoweza kuona kwamba sababu kubwa ya kujitolea kwake ilikuwa kwamba kizazi chake na kizazi kitakacho kuja baadaye kitakuwa chenye hofu ya Mungu na chenye kulindwa dhidi ya shetani mlaaniwa.

Tukilisoma tukio hili na matukio yanayofuata, tunajifunza kwamba baada ya kuzaliwa kwa Hadhrat Maryam (as), Mwenyezi Mungu alikubali sala za mama yake ambazo alisali kipindi akiwa mjamzito na kuweka thawabu kwa mtoto wake.

Zaidi ya hayo tunajifunza kwamba Mwenyezi Mungu alimteua Hazrat Zakaria (as) kuwa mlinzi wa Hazrat Maryam (as) ambayo inaonesha kwamba utaratibu huo huo unatakiwa ufanyike kwenye mpango wa Waqf-e-Nau kwa kuwa unafanana sana na tukio hili.

Kama Mwenyezi Mungu anavomtaja Hazrat Zakaria (as) kuwa mlinzi wa Hazrat Maryam (as), anaonesha pia kuwa, hili litawezekana tu kwa msaada wake.

وَّ کَفَّلَہَا زَکَرِیَّا ؕ کُلَّمَا دَخَلَ عَلَیْہَا زَکَرِیَّا الْمِحْرَابَ ۙ وَجَدَ عِنْدَہَا رِزْقًا ۚ قَالَ یٰمَرْیَمُ اَنّٰی لَکِ ہٰذَا ؕ قَالَتْ ہُوَ مِنْ عِنْدِ اللّٰہِ ؕ اِنَّ اللّٰہَ یَرْزُقُ مَنْ یَّشَآءُ بِغَیْرِ حِسَابٍ

*Na akamfanya Zakaria awe mlinzi wake. Kila mara Zakaria alipoingia chumbani kwake alikuta riziki pamoja naye. Akasema: Ewe Mariamu, unapata wapi hii? Akasema: Hii hutoka kwa Allah; hakika Allah humruzuku Amtakaye bila hesabu.* (3:38)

Kipindi Hazrat Mirza Tahir Ahmad (rh), Khalifa wa nne wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alipoanzisha mpango huu wa kimbingu, aliweka wazi muongozo kwa watu ambao watakuwa wasimamizi wa makuzi na malezi ya hawa watoto.

Kuna maelekezo mbalimbali yaliyowekwa kuwaongoza makatibu na waratibu wa mpango wa Waqf-e-Nau juu ya jinsi ya kuwaongoza Waqfeen-e-Nau baada ya wazazi wao kuwa wamewatoa kwa ajili ya kuhudumia Islamu na binadamu.

**Kutunza na kudumisha kumbukumbu**

Ni muhimu kwa makatibu na waratibu wote kufatilia idadi ya Waqfeen-e-Nau waliopo ambao wanawajibika kwao. Zaidi ya hayo, ni jukumu lao sio tu kutunza kumbukumbu ya idadi ya Waqfeen-e-Nau waliosajiliwa katika Jamaat zao bali pia kuendelea kuwakumbusha wazazi ambao wanataraji kupata watoto au waliooana kuwatoa watoto wao wajao katika mpango huu wenye Baraka.

Kwa muktadha huu, Hazrat Mirza Tahir Ahmad (rh) alisema katika hotuba yake ya uzinduzi tarehe 3 april 1987:

*"Ninataka kuwaeleza kwamba, idadi iliyopo ya watoto wa Waqfeen-e-Nau ni ndogo mno kuliko iliyotarajiwa. Kwa kweli, sio hata sehemu ndogo ya ilivyotarajiwa. Kwa kiasi nilicholiangalia hili suala, watu wenye wajibu wa kufikisha huu ujumbe kwa wanajamaat ni wa kulaumiwa kwa hili. Katika nchi kadhaa hawakupeleka ujumbe huu kwa wa Ahmadiyya wote"* (Hotuba ya Ijumaa, 3 April 1987)

***Katibu wa taifa anapaswa kuwajuza wana jamaat kwamba mara tu watoto wao wakishathibitishwa kuwa katika mpango wa Waqfu-e-Nau, wanapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kwake ili kuboresha kumbukumbu juu ya watoto hao.***

Hivyo basi, makatibu wote watatakiwa kuhakikisha kwamba wajumbe wote wana uelewa sahihi wa mpango wa Waqf-e-Nau na jinsi ya kuwatoa watoto wao.

Kuhusiana na hili, utaratibu ufuatao uzingatiwe:

**Jinsi ya kumtoa mtoto wako katika mpango wa Waqf-e-Nau**

Wakati wazazi wanatarajia kupata mtoto, wanabidi wamuandikie Huzoor Anwar (a.t.b.a) kumuelezea nia yao ya kumtoa mtoto wao katika mpango wa Waqf-e-Nau.

Maombi yanabidi yaandikwe kipindi cha ujauzito. Maombi yatakayofanywa baada ya kuzaliwa mtoto hayatakubaliwa.

Wazazi wote wanabidi waridhie maombi hayo yanayotumwa kwa Huzoor Anwar (a.t.b.a). Inapotokea kama mzazi mmoja sio mu Ahmadiyya, ridhio katika maandishi linahitajika kutoka kwake likieleza kuwa wanaelewa dhana ya kumtoa mtoto katika mpango huu.

Kwa sababu yeyote ile wazazi wakiamua kwamba watamtoa mtoto wa jinsia fulani tu, maombi yao hayatakubaliwa. Sio takwa kwamba mtoto awe wa jinsia fulani ndio atolewe kwenye mpango huu.

Ikishathibitishwa, mzazi anabidi atume kivuli cha nakala ya namba ya kumbukumbu (Hawala) ya Waqf-e-Nau ya mtoto wao kwa katibu wa eneo lake na taifa. Tangazo linabidi litolewe katika kila jamaat kwamba wazazi wawe na mawasiliano ya karibu na makatibu wa taifa.

Katibu wa taifa anapaswa kuwajuza wana jamaat kwamba mara tu watoto wao wakishathibitishwa kuwa katika mpango wa Waqfu-e-Nau, wanapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kwake ili kuboresha kumbukumbu juu ya watoto hao.

Katibu wa taifa wa Waqf-e-Nau anabidi aboresha kumbukumbu zake kwa taarifa zote zinazohitajika kuhusu mtoto. Mtiririko wa baadhi ya taarifa zinazobidi zitunzwe ni kama zifuatavyo:

**Kumbukumbu namba ya Waqf-e-Nau (Hawala)**
**Jina kamili**
**Jina la baba**
**Jina la mama**
**Jina la babu**
**Namba ya simu**
**Anuani**
**Mengineyo**

Katibu anapaswa mara zote awe analinganisha kumbukumbu zake na zile anazopewa na Markaz na kufanya marekebisho kwenye kumbukumbu zake ipasavyo. Kama kuna utata kwenye kumbukumbu, katibu anabidi awajuze Markaz.

*Endelea uk. 4*

# Muongozo kwa Wazazi wa Waqifiin-e-Nau

*Kutoka uk. 3*

Kama Waqf-e-Nau akiingia au kutoka kwenye Tajneed yake, ni jukumu lake katibu kuwajuza Markaz juu ya mabadiliko haya.
Katibu wa taifa anapaswa atunze kumbukumbu za maombi yanayosubiri na yale yaliyokishwapokea kumbukumbu namba.
Katibu wa taifa wa Waqf-e-Nau anapaswa kuanzisha madarasa ya lugha katika ngazi ya matawi, mikoa na taifa.

**Uanzishwa wa kamati za kupanga kazi**

Katibu wa taifa wa Waqf-e-Nau anapaswa aanzishe kamati ya kupanga au kushauri kazi kwenye ngazi ya taifa na mikoa. Anabidi aanze kupitia Waqfeen-e-Nau wote walio zaidi ya miaka saba. Watapata wazo juu ya vitu anavopenda mtoto na kisha watamuongoza uko katika miaka mingine ijayo.
Kwa hili, tunataka kukuvutia kwenye maelekezo ya Huzur Anwar (atba) kuhusu kamati ya kupanga kazi na kushauri kwa Waqfeen-e-Nau ambapo Huzur Anwar (atba) aliweka mkazo mkubwa katika yafuatayo:
Kamati inabidi ianzishwe katika ngazi ya taifa na pia katika matawi
Inaweza pia ikawepo katika ngazi ya mikoa kama jamaat ni ndogo ndogo na mbali mbali
Wajumbe wanapaswa wawe: Mwenyekiti – Amir wa nchi, katibu wa waqfeen-e-Nau wa taifa/ katibu ngazi ya tawi/ mbashiri, mwalimu, daktari, injinia, mwalimu kutoka Jamia kama jamia ipo kwenye nchi, na mtu yeyote mwenye uzoefu kwenye ushauri wa kupanga kazi. Ni juu ya kamati kumteua mjumbe mwingine yeyote. Kwa Waqifat, msaada utafutwe kutoka kwa Sadri Lajna kupitia kwa Amir au Rais wa jamaat.
Malengo ya hii kamati ni:

Kuwa na mtazamo wa jumla wa Waqfeen ambao wanakaribia kumaliza masomo yao

Kuwa katika nafasi ya kuwaongoza waqfeen kuhusu taaluma mbalimbali

Kujadili mahitaji ya baadae ya taifa lao na jamaat pamoja na kuona wangapi wanaweza kuchukuliwa na nchi yao, wangapi ni ziada na wangapi wanaweza kupatikana kwa ajili ya nchi zingine.

Kukusanya taarifa za za Waqfeen na walivyovifuzu, kiasi gani wanafaa kuhudumu au kuhifadhiwa au kupendekezwa.

Kuzipeleka mbele kwenye kituo kwa ajili ya kuyachambua zaidi maombi.

**Kuanzisha madarasa ya Waqf-e-Nau**

Madarasa ya kutoa elimu kwa Waqfeen yanapaswa kuanzishwa kufanyika mara moja. Taarifa za mawasiliano ya mwalimu zinapaswa kupelekwa ofisi kuu.
Madarasa haya yanabidi yafatiliwe na Murabbi husika wa jamaat. Mratibu anapaswa kumpa taarifa murabbi mara kwa mara.

**Ripoti za kila mwezi na kila mwaka**

Panga walau mpango mmoja au kikao amapo Waqfeen na wazazi wao watakuwepo. Wazazi wanaotarajia pia wanapaswa wawe sehemu ya mpango huu.
Ifanye mipango hii iwe na mwingiliano/husishi na iwe tofauti na mipango mingine yeyote ili wahudhuriaji wasichoshwe. Orodha ya wale wazazi ambao hawashiriki mipango hii licha ya kukumbushwa inabidi ipelekwe mbele ya ofisi kuu.
Vivyo hivyo, Ijtmai yam waka inapaswa ipangwe kwa ajili ya Waqfeen na wazazi wao ili waqfeen wajaribiwe juu ya uelewa wao wa elimu ya kidini na kidunia.
Makatibu wanapaswa kuwafundisha Waqfeen-e-Nau mtaala wa Waqf-e-Nau uliochapishwa na Markaz.

**Kuripoti**

Hakikisha unatuma ripoti mara nne kwa mwaka juu ya matukio yaliyofanyika kwenye mwaka huo. Unaweza kutuma mafanikio yeyote ya mtoto ili faili lake liweze kuboreshwa. Kuwa na mwasiliano na ofisi kuu mara kwa mara.
Ripoti zinabidi zitumwe katika vipindi vifuatavyo:

January mpaka Machi
Aprili mpaka Juni
Julai mpaka Septemba
Oktoba mpaka Disemba

Ripoti hizi zinabidi zipelekwe mbele ya katibu wa taifa wa Waqf-e-Nau. Ripoti pia zinabidi zikusanywe kutoka idara ya Waqf-e-Nau ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya na kurandanishwa na zile zinazotoka kwenye matawi, mikoa na taifa.
Ripoti zinabidi ziambatanishwe na picha kadri inavyowezekana.

**Kutembelea Markaz**

Mipango inabidi ifanywe ili Waqfeen na wazazi wao watembelee Markaz UK.

# Maarifa Juu ya Jahanamu na Peponi

Na **Musa Salum Mgeleka**
Dar es Salaam

*Sivyo! Lau mngalijua elimu ya yakini (ILMUL YAKIN):*
*Hakika mtaiona jahanamu:*
*Kisha hakika mtaiona kwa jicho la yakini (AINUL YAKIN):*
*Kisha kwa hakika mtaulizwa Siku hiyo juu ya neema (mlizopewa).*
Sura 102 : 6-9

*Na kama akiwa yu miongoni mwa watu wa kulia.*
*Basi ni salama kwako (ewe uliye) miongoni mwa watu wa kulia.*
*Na kama akiwa miongoni mwa waliokadhibisha, wapotevu,*
*Basi karamu yake ni maji yachemkayo.*
*Na kuwaka Motoni.*
*Bila shaka hii ndiyo haki yenye yakini (HAKKUL YAKIN).*
Sura Al-Waqi'ah 91 - 96

*Ili nifanye mema katika yale niliyoyaacha. Hapana! Hakika hili ni neno tu analolisema; na nyuma yao iko kinga (BARZAKH) mpaka siku watakapofufuliwa (UFUFUO).* [Surat Al-Mu'minun 101]

**Maarifa ya Pili Juu ya Jahanamu na Peponi**

Katika aya hizo Mwenyezi Mungu amebainisha kwamba waovu huwa na maisha ya kijahanamu katika dunia hii hii yanayofichikana; na kama wakitafakari wataishuhudia hapa hapa duniani. Hapa Mwenyezi Mungu ameigawa elimu katika madaraja matatu: Ilmul-Yakin (elimu ya yakini), Ainul-Yakin (jicho la yakini), Hakkul-Yakin (ukweli wa yakini). Ili kufafanua elimu hizi za namna tatu, mifano hii itasaidia: Kwa mfano, mtu akiuona moshi mwingi kutoka mbali, mara fikira yake kutoka moshi itaelekea kwenye moto na atakuwa na yakini kuna moto huko kwa kufikiria kwamba kuna uhusiano usiotanguka baina ya moshi na moto, na kuna ufungamano kamili kati yao; penye moshi pana moto. Basi elimu hii huitwa Ilmul-Yakin, yaani yakini iliyopatikana kwa njia ya hoja na dalili, siyo kwa kukiona kitu hasa. Na kisha akiisha uona ulimi wa moto atapata Ainul-Yakin, yaani jicho la yakini au tuseme yakini iliyopatikana kwa kujionea kitu chenyewe. Kisha akiingia mwenyewe katika moto atapata Hakkul-Yakin, yaani ukweli wa yakini — yaani siyo ameona tu kwa macho bali ameisha athirika na hicho. Basi, Mwenyezi Mungu anasema katika aya hizo kwamba elimu ya yakini ya Jahanamu mwaweza kuipata katika dunia hii hii; kisha huko katika Barzakh mtapata Ainul-Yakin, na siku ya kufufuliwa elimu yenu hiyo itafikia daraja la Hakkul-Yakin.

Ibainike hapa kwamba sawa na mafunzo ya Kurani Tukufu, ziko aina tatu za ulimwengu.

Kwanza, dunia iitwayo ulimwengu wa vitendo na uumbaji wa kwanza. Katika dunia hii mtu hutenda mema na maovu. Ijapokuwa huko akhera pia maendeleo yatapatikana, lakini hayo ni kwa fadhili ya Mungu tu wala siyo kwa juhudi za mtu.

Ulimwengu wa pili huitwa Barzakh. Kwa hakika katika lugha ya Kiarabu Barzakh ni kitu kilichopo baina ya vitu viwili. Na kwa kuwa zama za baada ya kufa ziko baina ya dunia hii na akhera, basi zikaitwa Barzakh. Neno hili tangu kale tokea kuumbwa kwa dunia hii linatumika kwa ulimwengu wa kati, kwa hiyo ndani ya neno hili ushuhuda umefichikana juu ya kuwepo kwa ulimwengu wa katikati.

Barzakh ni neno la Kiarabu lililo mchanganyiko wa Zakh-kha na Barra, maana yake nafasi ya kutenda matendo imekwisha na ikaingia katika hali ya uficho. Hali ya Barzakh ndiyo ile ambapo umbo hili la muda la binadamu linavunjika, na roho na mwili hutengana. Jinsi mwili unavyowekwa katika shimo (kaburi) ndivyo roho nayo inavyoingia katika shimo la aina fulani linalohakikishwa na neno Zakh-kha, kwani sasa haiwezi kutenda mema au mabaya yaliyowezekana kwa kuungana mwili na roho.

Yafaa kuzingatia kwamba Mwenyezi Mungu Amemwumba mtu kwa ajili ya kupata maendeleo yasiyokoma Surah 22:6. Basi kama mtu hawezi kupata maendeleo katika maisha haya mafupi bila ya kuwa na mwili, tutumainije kupata maendeleo yasiyo na mipaka vivi hivi bila kuwa na mwili?

Basi yathibitika kutokana na dalili hizi kwamba sawa na kanuni ya Kiislamu haina budi roho kuwa na mwili kwa kudumu ndipo iweze kutenda matendo kamili. Ingawaje baada ya kufa mwili huu wa kuangamia hutengana na roho, lakini katika hali ya Barzakh kila roho huazimiwa mwili mmoja ili kuionjesha kidogo matokeo ya amali zake. Mwili huo haufanani na mwili huu; bali huo huumbika kutokana na nuru au giza sawa na vitendo vya mtu, kana kwamba katika ulimwengu huo wa Barzakh, vitendo vya mtu hufanya kazi ya mwili. Ndivyo ilivyoelezwa mara kwa mara katika Neno la Mungu; na baadhi ya miili imesemwa

*Inaendelea uk. 11*

# Uongozi katika Islam

*Kutoka uk. 1*

wake kama mwanamke. Mwanamke anamajukumu ya kumsaidia mmewe kumuangalizia nyumba, kutunza watoto wake, kuwalea na kuwafunza adabu na dini. Na jukumu lilolo kubwa zaidi kubeba ujauzito. Ujauzito huchukua takriban miezi 9 na kunyunyeshankwa muda mrefu ni miaka 3 hapa ni sawa na miaka 4 na muda wote huu wa miaka minne mwanamke anakuwa dhaifu kufanya kazi hata uhakika wa mapato.

Hivyo Familia zingekufa kwa maana mbili. Moja - Kukosa Malezi bora ya wazazi kwa kumfanya mwanamke atafute kwa bidii sawa na mwanaume. Mbili - Kimapato yasingetosha ikiwa mwanamke akatimiza wajibu wake.

Mwanaume akafanywa kuwa Kiongozi na sio Bora mbele ya Allah ili tu Atimize wajibu wake huu adhimu na ili Familia istawi kwa adabu na uchumi.

Maungano ya Ndoa yasingekuwa na Kiongozi basi Mapenzi na Taqwa isingekuwepo. Mapenzi ni haya Upande mmoja ni Kutoa na Upande Mwingine ni Kutii kiukweli kama hakuna njia hii ya Kutoa na Kutii Mapenzi hamna.

Ni nani awe kiongozi basi mwenye Majukumu mengi zaidi ya mwenzake na ndiye anapaswa pia kutoa na Mwanamke atii. Na katika dhana hii ndipo Mtume s.a.w alisema kama angeamuriwa mtu kusujudia mtu mwingine basi mwanamke angemsujudia mwanaume hii kwa sababu ya majukumu haya tu na ndivyo Mtume s.a.w alipoulizwa ni nani anapaswa Kunyenyekewa zaidi alijibu Mama, Mama, Mama, kisha Baba. Huzur V atba anasema ni kwa sababu Mama ana majukumu mengi zaidi kwa watoto zaidi ya Baba na ni Kiongozi wao.

Sababu nyingine ya kwa nini Mwanaume ni Kiongozi juu ya Wanawake ni ya Uumbaji. Yaani wanawake wameumbwa Dhaifu zaidi ya Mwanaume. Udhaifu huo unawafanya kuwa na uwezo mdogo wa kuwaongoza wanaume

Mtume s.a.w anasema: watunzeni wanawake vizuri. Kwani mwanamke ameumbwa kutokana na Ubavu (yaani tabia yake imepindamana). Na mfano wa ubavu huwa unapindamana zaidi katika sehemu ya juu. Mkijaribu kuunyosha mtauvunja. Na mkiubakiza katika hali yake utabakia katika hali ya kupidamana (na mtafaidika nao). Basi waangalieni wanawake vema

Udhaifu hupatikana kwa siku zake za Hedhi, Mimba, Kuzaa, Kunyonyesha na Kutoridhika

N.k

Siku hizo uwezo wa mwanamke kufikiri na kutoa maamuzi ya busara hushuka. Na ukifatilizia sana kwenye ndoa maugomvi mengi huibuka kwa kasi katika siku za Hedhi za mwanamke, Mimba, Kuzaa yaani kuwa na mtoto, Kunyonyesha n.k na hivyo huibua mambo mengi yasiyo na uwezo wa kufikirika na kutekelezeka.

Mtume s.a.w alisema Mwanamke anabahati mbaya sana maana awapo kwenye Hedhi Hasali na kipindi hicho hushambuliwa sana na Shetani. Hivyo akawaomba sana kujitahidi Kuomba Maghofira, Kumkumbuka Allah zaidi na Kutoa Sadaka

Uongozi huhitaji umakini na maamuzi ya Hekima hivyo Akakabidhiwa Mwanaume

Sababu nyingine ya Uumbile ni kwa Wanaume wakafanywa wakamilifu zaidi ya Uumbaji zidi ya wanawake kwa sababu hizo zote juu ili waweze kubeba majukumu yao ipasavyo na Kuwasaidia kuondoa Udhaifu wa wanawake.

Kiongozi huwa kamili zaidi ya anawaongoza maana huchaguliwa kutoka miongoni mwetu. Na hali yake husaidia udhaifu wa wengine

# Historia yaandikwa tawi la Jamaat Ahmadiyya Chanika

**Na Mwandishi Wetu**



*Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akiongoza uwekaji wa jiwe la msingi katika msikiti wa Chanika.*

Tarehe 16.08.2020, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania aliongoza uongozi wa Jamaat wa mkoa wa Dar kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa msikiti katika tawi la Chanika jijini Dar es salaam.

Akieleza malengo ya msikiti, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliwataka wanajamaat wote kuutumia msikiti kwa ajili ya ibada na kuwa kituo muhimu cha malezi.

Ujenzi huo utakaochukua miezi miwili kukamilika ni miongoni mwa misikiti mipya inayojengwa mkoani Dar es salaam, mingine ile ya Tegeta na Vikindu.

Akimueleza Amir sahib, Rais wa tawi la Chanika Dr. Swaleh Pazi, alimuahidi Amir sahib kusimamia ujenzi huo kwa karibu na kushirikiana kila hatua ili kupata msikiti mzuri na wenye viwango vinavyokubalika na Jamaat.

Wengine waliohudhuria katika hafla hiyo ni Naib Amir Issa Mwakitalima, Sheikh wa Mkoa, Sheikh Nadeem Ahmed, Katibu Mkuu wa ziada Sheikh Abdulrahman M. Ame, Sheikh Basharat Rehman, Rais wa Jamaat Mwanza Yahya Kambaulaya na viongozi wa tawi la Kitonga na wageni waalikwa.

Mwisho Amir Jamaat aliongoza maombi ya kufunga hafla hiyo fupi.



# Maisha ya Mtume Muhammad s.a.w

*Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili*

Zile zama alizozaliwa Mtume Mkarimu Muhammad s.a.w. zinapaswa pia kufahamika kuwa ni sehemu ya maisha ya Mtume s.a.w. kwa sababu kwa kuzitilia maanani hali hizi hizi, mtu anaweza kuzifahamu vyema hali za maisha yake.

Yeye alizaliwa Makka na kuzaliwa kwake kunaafikiana na mwezi wa Jua wa August mwaka 570. Jina alilopewa wakati wa kuzaliwa lilikuwa ni Muhammad lenye maana ya Aliyesifiwa.

Wakati alipozaliwa, takriban waarabu wote wa zama hizo, ukiacha wachache, walikuwa ni washirikina. Watu hawa walikuwa wakijisema kuwa ni wazao wa Ibrahim na pia walikuwa wakiamini kuwa Ibrahim hakuwa mshirikina. Lakini juu ya hayo, walikuwa wakifanya ushirikina na walikuwa wakitoa dalili hii, kwamba baadhi ya wanadamu hupata maendeleo kiasi hiki kwamba huupata ukaribu sana na Mwenyezi Mungu kiasi ya kwamba maombezi yao hukubalika tu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na kwa kuwa dhati ya Mwenyezi Mungu ni yenye shani ya hali ya juu mno, inakuwa si uwezo wa kila mtu kufika huko. Ni mtu tu aliyekamilika awezaye kufika hadi huko, hivyo ni muhimu kwa mtu wa kawaida atafute wasila na aombe radhi na msaada wa Mwenyezi Mungu kupitia wasila huyo.

Kwa mtazamo wa itikadi hii ya ajabu, juu ya kumuamini Hadhrat Ibrahim a.s. kuwa ni mtu aliyekuwa na imani ya Umoja wa Mwenyezi Mungu, bado wakawa wanajijengea dalili ya ushirikina (wakisema); Ibrahim alikuwa ni mwema mno, yeye alikuwa na uwezo wa kufika moja kwa moja hadi kwa Mwenyezi Mungu, lakini watu wa Makka hawakuwa na daraja hilo. Ndio sababu walikuwa na haja ya kuwafanya baadhi ya watakatifu kuwa wasila.

Walikuwa wakiyaabudu masanamu ya watakatifu hao kwa ajili ya kupata kusudio hilo, na kwa namna hii walidhani kuwa wanawafurahisha (watakatifu hao) na kuwafanya wasila (waombezi) wao mbele ya Mwenyezi Mungu.

Akili zao hazikuelekea asilan kwenye utatuzi wa kasoro na hitilafu zilizomo ndani ya itikadi hii, kwa sababu wao hawakuwa na mwalimu wa (kuwafundisha) umoja wa Mungu. Ushirikina uanzapo ndani ya kaumu yoyote, basi huwa unaendelea kukua. Moja huwa mbili na mbili huwa tatu. Hivyo wakati wa kuzaliwa kwa Mtume s.a.w., sawa na kauli za wanahistoria, kulikuwa na masanamu 360 ndani ya Kaaba (ambao kwa sasa ndio msikiti mtakatifu wa Waislamu na nyumba ya ibada iliyojengwa na Hadhrat Ibrahim na Hadhrat Ismail a.s.). inakuwa kana kwamba sawa na kalenda ya mwezi kila siku ilikuwa na mungu wake tofauti.

Mbali na masanamu haya, kwenye miji mikubwa mikubwa ya jirani na kwenye makao makuu ya watu, kulikuwa na masanamu tofauti, kana kwamba Bara Arabu ilikuwa imekumbwa na ushirikina kila mahala.

Waarabu walikuwa wakijali sana ustaarabu wa lugha yao na kuiboresha. Walijitahidi sana kuifanya lugha yao iwe ya kielimu lakini mbali na hiyo, elimu haikuwa na maana yoyote kwao. Hawakuwa na elimu yoyote waliyoijua iwe ya Historia, Jiografia, Hesabu n.k. Naam, kutokana na kuishi kwao jangwani na kusafiri kwao humo, wakawa mabingwa wa elimu ya nyota. Hakukuwa hata shule moja Bara Arabu yote. Inasemwa kwamba huko Makka kulikuwa na watu wachache sana waliokuwa wakijua kusoma na kuandika.

Kuhusiana na maadili, watu wa Arabuni walikuwa ni watu wenye mielekeo ya ajabu ya pande zote mbili. Baadhi ya dhambi za hatari mno zilipatikana miongoni mwao na mlipatikana pia baadhi ya mema ambayo yalinyanyua mno kiwango cha wema cha watu wao.

# Bustani ya Washairi

**KUBETI**

1. Imeshakua fasheni, kufanya yaso na mana
Najiuliza kwa nini, wanapotoka Vijana
Hamsikii kwa nini?, kamari iwe hapana
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

2. Kamari iwe hapana, isichezwe majumbani
Kukopa hela hakuna, sifanye ufirauni
Si usiku si mchana, mnajazana kumbini
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

3. Mnajazana kumbini, mnashindwa kupishana
Kutafuta milioni, mwaka mzima hakuna
Hamuoni hata soni, fanyeni kazi vijana
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

4. Fanyeni kazi vijana, mikeka ya kazi gani?
Mara kepu mara chana, una mkosi jamani
Badilika embu ona, unasubiria nini?
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

5. Unasubiria nini, kufanya vyenye maana
Muda mali kama nini, nakukumbusha kijana
Usije kuwa mgeni, wenzako wameshaona
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

6. Wenzako wameshaona, kamari ni ushetani
Embu fikiri kwa kina, ni mbaya kama ugoni
Na vijiwe vya mchana, mara baka mara mani
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

7. Nimeshafika mwishoni, nimesema vyenye mana
Jikiteni masokoni, pambana bado kijana
Msigande vibandani, kumuua barcelona
Tuendako si kuzuri, mnapotea vijana.

**Abdallah Kalindima (K-mtoto)**
+255 717 936 353,

**UZURI HASA**

Kwa jina Lake Kahari, ndilo ninalotamka
Anijalie khairi, niweze kueleweka
Niifikishe khabari, pale panapotakika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kitu hupata uzuri, ukawa wa kusifika
Na tena ulo dhahiri, pote pote unawaka
Hakika unaathiri, na pia hauna shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kama chakula sukari, utamu inasifika
Ailaye hudhihiri, hii tamu ya hakika
Utamuwe huathiri, ulimi husisimka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Huwa hanayo habari, homa inapomshika
Kuwa ni tamu sukari, mdomoni ikifika
Moyo wake ukihiri, na mara huitapika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Mtume mwenye fakhari, Muhammadi katamka
Husuda tujihadhari, wemani tutaondoka
Sababuni kama nari, kwenye kuni ikishika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Muhamad kadhihiri, ushahidi uso shaka
Na kwa mengi matabiri, vitabu vya kablika
Vilieleza dhahiri, ni Nabii wa Rabuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Japo Mola Kahari, Kasema ni msifika
Vitabu vimekariri, ni mkweli aso shaka
Lakini watu jeuri, tafakuri likakuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Hoja wakatahayari, kukosa la kutamka
Wakaipanga shari, ya mauti kumfika
Ikabidi ahajiri, Madina kutoka Maka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Ndivyo alivyodhihiri, Ahmad kwa hakika
Ushahidi wa Bukhari, Muslim kadhalika
Quran yakariri, Manabii watafika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Yeye kwa kudhihiri, dini imeimarika
Bidaa zilokithiri, zenyewe zinatoweka
Ya Muhamadi athari, inabidi kung'arika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Twangalie kwa ari, husuda kuiepuka
Ndio hasa kwa dhahiri, wema wetu hufunika
Tukashindwa jua siri, Nabii aliyefika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Tumuombe ya Kahari, Mola Aliyetukuka
Atujuze hiyo siri, ya Nabii Msifika
Na tena Atusitiri, tukubali pasi shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

**Hassan Sango (Jange Muqadas, kwenye karatasi)**
Dar es salaam

**KIFO.**

HU! Japo kina umiza, Ndo hivyo hakikwepeki,
Chabaki kutushangaza, Wala hakitabiriki,
Mioyoni hudumaza, Kifo hakiombeleki,
Dah! Kifo cha huzunisha, Pia na kusikitisha.

Jamani inaumiza, Pindi kinaposikika,
Twa baki twa jiuliza, Kama kina epukika,
Kifo cha tujaliliza, Hofu na kuweweseka,
Mmmh! Kifo cha huzunisha, Kifo kifo tusamehe.

Nacho pia kiliumbwa, Kwa kutumaliza sisi,
Watu wote tutakumbwa, Kutengana zetu nafsi,
Ardhi nyingi zitachmbwa, Na tutaingizwa sisi,
Tena kweli kifo kipo, Hakuna kujidanganya.

Lo! Kifo hakibagui, Si mkubwa si mtoto,
Umbile hakichagui, Kipo hata kwenye joto,
Kinapokuja hujui, Kifo kama ka la moto,
Kifo hakina huruma, Yeyote cha Mchukua.

Cha sababishwa kwa mengi, Ajali magonjwa pia,
Tena cha ondoa wengi, Wabakiao walia,
Na cha sababisha mengi, Maumivu kutwachia,
Kifo si tumeumbiwa, Twa subiri chukuliwa

**Abubakary Abdallah Mwita**
**Mkurya harisi**

**NDIYO MAPENZI YA MUNGU**

Hongera kwa Muhariri, Kunitengea nafasi
Nami nipate dhukuri, Nitaruku nafsi
Niimbe langu shairi, Kwa wino na karatasi
Gazeti kufika leo, Ndio Mapenzi ya Mungu

Mungu akitaka jambo, hulitengea nafasi
Kisha akalipa umbo, Akalivisha libasi
Na kulitia urembo, Unyayo hadi utosi
Limedumu hadi leo, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Tangu lianze safari, Ni mbali sana kitambo
Miongo sasa dahari, Bado limeshika fimbo
Kama wimbi la bahari, Meli huzipiga kumbo
Hebu leo litajeni, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Sikuwepo siku zile, kiroho hata kiumbo
Ni wengi walisomile, Hili gazeti la tambo
Ndipo nasema simile, Enyi wajuzi wa mambo
Someni mlirudile, Ndiyo Mapenzi ya Mungu.

Gazeti lenye haiba, Nguvuze bado zitele
Bado linabeba huba, yake tumwa mteule,
Hadi hapo msalaba, ung'oke utoke pale
Tuunganike kwa hili, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Gazeti la mahubiri, Tangu zama za kale
Gazeti la washairi, Hasa wale wateule
Kina Akili si Mali, Akina Mpukutile
Wengi walipita shule, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Na mimi nilikutile, Gazeti la siku tangu
Likanibeba kwa lele, kukarimu tungo zangu
Miaka sasa itele, ni nyeupe nywele zangu
Gazeti Mwalimu wangu, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Wakatabu kalamu, nafupisha tungo yangu
Ingawa bado na hamu, kubarizi na wenzangu
Lakini yanilazimu, niwapishe na kwa tungu
Kusoma gazeti hili, Ndiyo Mapenzi ya Mungu.

**A.R Mikila (SIASA)**

**SHAMBA ULICHAGUE**

1. Kwa mola nakimbilia, ardhi alotandaza,
Matunda nayo mimea, tele akavieneza,
Ichague pakumea, parutuba tosheleza,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

2. Shamba bora kuchagua, si rangi lilokoreza,
Rotuba liloivia, si nyeusi kuteleza,
Unyevu unotulia, si kame la kuumiza,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

3.Shamba kulihudumia, nyasi gugu kupunguza,
Samadi nayo mbolea, rotuba ukaijaza,
Udongo pate ivia, unga'e na kupendeza,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

4.nyama na hiyo mimea, mboji kuitengeneza,
Nafaka kunde fukia, ardhi kuendeleza,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

5.mbegu bora kichagua, fukia pakupendeza,
Kisha Maji mwagilia, kiasi kutosheleza,
Na dawa ipulizia, zuia kuambukizwa,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

6.shamba bora kichagua, mazao yatapendeza,
Chapu chapu yatakua, matunda kujitokeza,
Mavuno tafurahia, wala shida hutowaza,
Shamba ukilichagua, zao jema utavuna.

7.ewe wahhab jalia, shamba la kunipendeza,
Shamba lililotulia, mola lenye kumuwaza,
Lipate kunizalia, kwa Allah chakukiuza,
Shamba ukilichagua, zao bora utavuna.

**Masihi Omary Kisagwa**

**HABA JANA**

Rabu nashika Kalamu, Kichwani tenzi sina
Kuidondosha haramu, Vidole vinakwazana
Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

Safari nimeianza, Navuta pumzi joto
Kauli zinanipinza, Pekua njia kokota
Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

Weka hatua Jasiri, Sauti mwangwi yanadi
Shari siriye safari, fumbo ongeza juhudi
Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

Kusafiri sina budi, umuhimuwe najua
Wengi waacha kusudi, ili tushindwe ng'amua
Hino safari Waqfu, Ni ngumu tundale tamu

**Shunda Mshundia Wana**
Daluni, Tanga
+255656557721

**HOJA BORA**

Kwa mateka na viboko, huwezi kujibu hoja
Mwendo uso na mashiko, aula chembe ya tija
Hilo hasa ni chimbuko, la kutoweka faraja
Ni hoja iliyo bora, kufuta ile dhaifu

**Mahmood Hamsin Mubiru** (Wa Mamba)

# Mkutano wa Wanyama

Mfalme simba alikuwa ametingwa na shughuli ya kuwateua wanyama mbalimbali katika nafasi mbalimbali huko himayani. Duma alichaguliwa kama kamanda wa jeshi kwa sababu alikuwa mwepesi kufikiria na mkimbiaji hodari kuliko yeyote. Tembo mwenye busara alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa himaya ya wanyama.

Muda ukaendelea kupita na wanyama wengine pia wakapata nafasi zao. Hatimaye, sungura, kobe na bunda pekee ndio wakabakia. Basi ajabu, wanyama wakaanza kucheka. Pundamilia akasema,



"Sungura anatishika kirahisi na kobe naye huchukua saa kadhaa kujongea kaumbali kadooogo. Punda naye ni mpumbavu. Hawawezi kupata nafasi za kutumikia katika baraza la mfalme."

Lakini simba mfalme akasema, "Hapana rafiki, msiwatanie. Wanyama wote wana uwezo tofauti na wa kipekee. Sungura atakuwamjumbewetukwasababuanakimbia haraka haraka. Kobe naye anaweza sana kujificha na kuchunguza kwenye mipaka ya himaya yetu. Sauti kubwa la punda linaweza kutumika kama mbiu." Wanyama wote wa msituni walijifunza somo jipya siku ile.

. . . . . .

Fundisho: Tunatakiwa kujifunza kumheshimu kila mtu.

# TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

| | | | |
|---|---|---|---|
| Dhambi | Uanadamu | Dini | Ubaguzi |
| Maarifa | Ushari | Maezi | Ushujaa |
| Uaminifu | Dhuluma | Ubadhirifu | Elimu |
| Usengenyaji | Majaribu | Ushirikiano | Mama |
| Deni | Ubabe | Dunia | Ubakhili |
| Mahaba | Ushirika | Mali | Ustaarabu |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | U | L | U | B | A | D | H | I | R | I | F | U | M | C | M |
| R | U | B | A | K | H | I | L | I | U | M | A | L | E | Z | I |
| U | V | R | A | M | I | U | R | K | S | M | T | Y | Q | B | D |
| N | A | T | U | B | R | D | B | W | E | I | B | B | U | V | U |
| M | X | M | M | S | E | D | K | A | N | K | L | Q | S | U | N |
| N | U | A | I | V | T | R | K | I | G | L | Q | N | H | S | I |
| U | H | S | R | N | U | A | D | T | E | U | K | F | A | H | A |
| D | A | V | H | M | I | Z | A | R | N | K | Z | D | R | U | U |
| L | R | N | I | I | Z | F | P | R | Y | D | F | I | I | J | S |
| V | F | L | A | C | R | A | U | M | A | A | R | I | F | A | H |
| L | E | R | D | D | M | I | F | K | J | B | J | V | Y | A | I |
| Z | V | H | F | U | A | I | K | I | I | Z | U | F | M | F | R |
| T | Z | B | L | T | L | M | N | I | P | M | A | M | A | K | I |
| L | Q | U | L | A | Z | E | U | M | A | H | A | B | A | M | K |
| Z | H | N | M | X | D | K | H | W | V | N | K | F | P | W | A |
| D | M | A | J | A | R | I | B | U | H | V | O | F | Q | M | Q |

# UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



# Kupika Maandazi ya Saga Noti

Na **Mtandao**



**Mahitaji ya donge la sukari:**

- Unga vikombe 3 - Maziwa kikombe 1 ya vuguvugu - Sukari nusu kikombe - Hamira kijiko 1 - Yai moja - Samli vijiko 2 (sio lazima)

**Mahitaji ya donge la sukari:**

- Unga vikombe 3 - Maziwa kikombe 1 ya vuguvugu - Chumvi nusu kijiko - Samli vijiko 2 (sio lazima) - Yai moja - Hamira kijiko 1 - Mafuta ya kuchomea

**Mahitaji ya shiira:**

- Sukari kikombe kimoja na nusu - Maji kikombe 1 - Hiliki ya unga kijiko 1 au vanilla.

**Jinsi ya kutayarisha**

Changanya vitu vyote vikavu vya unga wa sukari tia maziwa uponde mpaka uwe laini weka kando. Chukua vitu vyote vikavu vya Unga wa chumvi changanya tia maziwa uponde mpaka uwe tayari. Chukua donge la chumvi sukuma duara kama chapati weka kando chukua na donge jengine la sukari sukuma kama chapati halafu weka chapati moja chini ya chumvi na uweke wa sukari juu yake halafu ziroll pamoja Halafu katakata size ndogo ndogo kwa kutumia uzi au kisu kikali fanya hivo hivo mpaka umalize wacha ziumuke choma kwa mafuta kama maandazi kwa moto wa kiasi.



Pika shira kama ya kaimati iache ipoe halafu zitie kwenye shira zipakaze na shira ienee vizuri,tayari kuliwa.



## ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

### Umoja wa Mungu

Umoja wa Mungu ni nuru iuangazao moyo baada ya kukatalia mbali miungu yote, iwe ni miungu ya dunia ya ndani au dunia ya nje.

Huifunikiza kila chembe ya nafsi ya mtu. Hali hii yawezaje kupatikana bila msaada wa Mwenyezi Mungu na kumfuata Mtume Wake? Wajibu wa mtu ni kujiua nafsi yake na kuyapa kisogo majivuno ya kishetani.

Asijigambe eti amelelewa kwenye kao la elimu, bali yuwapaswa kujihesabu kuwa mtu asiyejua cho chote, na kudumu katika maombi.

Ndipo nuru ya Umoja wa Mungu itamshukia na kumpatia maisha mapya.

(Rhoohani Kazain Jal. 22, Uk. 148: Hakikatul - Wahyi Uk. 144)

# DARASA LA QUR'AN TUKUFU

## Tofauti kati ya Hatia na Dhambi

Na **Musa Salum Mgeleka** - 0717 504 690

(وَمَنْ يَكْسِبْ خَطِيئَةً أَوْ إِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهِ بَرِيئًا فَقَدِ احْتَمَلَ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُبِينًا)

[Surat An-Nisa' 113]

Surah 4:113

*Na mwenye kufanya hatia au dhambi, kisha akamsingizia nayo asiye na kosa, basi kwa hakika amebeba masingizio na dhambi iliyo wazi.*

**Khatiiah - hatia** ni kosa linalofanywa ama kwa kukusudia au bila kukusudia na linamhusu mwenyewe aliyelifanya. Na **ithmun - dhambi** ni kosa linalofanywa makusudi na linaweza kuenea kwa watu wengine pia. (Aqrab, Mufradat na Lane).

Sawa na maana hizo hatia ni kosa la makusudi au bila makusudi wakati dhambi ni kosa la makusudi. Hatia ni kosa kinalofanywa na mtu mwenyewe wakati dhambi inafanywa na mtu mwenyewe na wengine. Mfano kwa makosa yenyewe;

Uwongo ni hatia maana kwa namna ya mwanzo uwongo hutendeka kwa mtu mwenyewe. Ila kama uwongo unaweza kufanya mwingine kufanya kosa basi uwongo unakuwa dhambi. Uzinifu ni dhambi na sio hatia kwa kuwa hufanywa na mtu zaidi ya mmoja.

Hatia hufanywa kwa kuwa na hisia ya uovu. Mfano ibilisi alifanya hatia au kosa la kutotii kwa sababu ya **ukafiri** 2:35 na **kiburi** 7:14 na hii inamaana sifa hizi za ukafiri na kiburi ndio humwingiza mwanadamu kwenye hatia na sifa hizi yeyote anaye zimiliki na zikimtawala bila shaka ataingia hatiani tu.

Dhambi hutendeka kwa uwepo wa hatia na mwenye hatia hutia ushawishi kwa wengine ili kutenda dhambi au makosa. Ibilisi alipofanya hatia aliweka mikakati ya kuwashawishi wengine kuingia kwenye uovu 7:15-19 na kitendo cha ushawishi kikaitwa shetani 7:21 na shetani hutumia **udanganyifu** kushawishi kuingia kwenye dhambi 7:22-23, udanganyifu ni katika kutamani vitu vya dunia 31:34 na kushika ukafiri 67:21

Hatia na dhambi zote ni uovu na kila uovu una hukumu yake na adhabu zake. Dhambi ni mbaya zaidi ya hatia maana inafanya uovu au makosa kuendelea. Dunia ina sheria na magereza ya kuzuia **hatia** na kila mwenye makosa akihesabika mwenye hatia pekee. Wakati mmoja mzinifu atahukumiwa ama mwanaume au mwanamke pekee, muuaji atahukumiwa anayeuwa tu bila kuangalia aliyesababisha kuuwa. Namna hii haiondoi makosa na kuacha mbegu nyingi mutaani ya uovu isiyotibika na mbegu hiyo huendelea kuzaa uovu mwingine. Islamu inafundisha mfanya kosa na msababishi wa kufanyika kosa wote wanaahabu zao 24:3 na desturi ya mahusiano baina ya watu yategemee kiwango chao cha imani yaani muovu na muovu washirikiane na mwema kwa mwema 24:4 na usifanye urafiki na makafiri na maadui zako. Lengo hapa ni kuzuia uovu kuenea na kuwepo makusudi ya kurekebisha tabia kwenye kada zao. Hatari ya kuwachanganya ni rahisi zaidi kwa wema kupotea kuliko wema kuwabadili waovu. Malaika na ibilisi walipoamriwa kumtii Nabii Adam as ila ibilisi **aligoma kutii** 7:12-13 na ibilisi alipogoma kwa uasi wake aliamriwa na aondoke kwenye himaya ya nabii adam as 7:14. Ila pia Nabii Adam as akatahadharishwa kukaribia jamii ovu 7:20 na alipoikaribia naye akaondolewa sehemu takatifu 7:21-23 na 25-26

Tofauti hizi zipo ili kujitathimini juu ya namna ya matendo yetu tunavyo yaendea ili kuepukana na makosa ya aina ya hatia na dhambi ili siku ifike jamii yetu kushika wema, Inshaallah.

Tunamuomba Allah Atuepushe na kila viashiria vya maovu. Amin

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Banda la Tabligh la Tanzim ya Ansarullah katika eneo la Kigamboni, hatua chache toka kivuko cha pantoni*



*Mhe Amir na Mbashiri Mkuu aliweka Jiwe la msingi la Msikiti mpya katika tawi la Chanika mkoani Dar.*




*Moja ya mabanda ya Tabligh ya Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya mikoani*



*Mbashiri wa Arusha, Sheikh Muhammad Shafi Memon akimpa mheshimiwa Anna Mgwira zawadi ya vitabu aliposhiriki maonyesho ya Nanenane jijini Arusha 2020.*




*Wanafunzi wa Jamia walifikisha ujumbe wa Islam Ahmadiyya katika Maonyesho ya Vitabu katika Nanenane 2020 mkoani Morogoro.*



*Wanajumuiya wakijitolea walifanya Waqar-e-Amal katika msikiti. Mwanza, Tanzania*



*Tarbiyyati Class mkoa wa Shinyanga 02 Aug - 15 Aug*



*Wanajumuiya walifanya Waqar-e-Amal kwa ajili ya kujenga ukuta wa maeneo ya msikiti. Songea, Tanzania*



*Tawi jipya la Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mkoani Dodoma limeanzishwa. wanajumuiya wanasali sala chini ya mti. kuanzia sasa wameanza maandalizi ya ujenzi wa Msikiti.*
*Mwenyezi Azibariki juhudi zao, Awajaalie uthabiti wa imani na moyo. Amin*




*Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na Sadr Khuddam katika ufunguzi wa Wakal Amal Masjid Salaam*



*Tarbiyyati Class kwa matawi ya Kitonga, Jalsa Gah na Qadian ya jijini Dar es salaam.*
*Darasa hili la malezi lilifanyika katika msikiti wa uliopo maeneo ya Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya.*

# Bwana Sheikh Abdul Qadir

## Mwandishi wa "Maisha Matakatifu"



**Sheikh Muzaffar Durrani**
Rabwah, Pakistan

Sheikh Abdul Qadir alizaliwa tarehe 15 Agosti 1909 katika nyumba ya Mbaniani Khatri huko Gorana Pathanan, Kata ya Bhalwal, wilaya ya Sargodha. Wazazi walimpa jina Sodagar Mal. Baba yake Lala Wazir Chand aliwezaje kujua kwamba mtoto wake anayeitwa Sodagar Mal kulingana na biashara yake, katika zama zijazo atakuwa mwana biashara wa kiroho kwa kutumikia Islam na siku itawadia atakapoongoza wengi.

Sodagar Mal alipata masomo ya awali katika kijiji chake. Alihitimu masomo yake ya kati katika shule ya kati ya Lalian, Wilaya Sargodha. Masomo ya mbele bado yalikuwa katika mazungumzo, katika hali hiyo alihamia kwa familia yake Dhakhira Beranwala, kata ya Hafidh Abad, wilaya ya Gujaranwala kutoka wilaya ya Sargodha, alisaidia katika biashara ya familia, katika hali hiyo Mungu Alimfungulia mlango wa Islam. Ilitokea hivi kwamba Katika kijiji kile kile cha kata ya Hafidh Abad ambapo alikuwepo Sodagar Mal, kijana mzuri Mbaniani, humo humo alikuwepo mwenye duka Mian Muhammad Murad, Mwislamu Mwaahmadiyya aliyetambulika kwa uzuri na ukweli wake mpaka mbali.

Sodagar Mal na sasa Sheikh Abdul Qadir alijuana na Mian Muhammad Murad. Yeye akiona alama ya mwongozo na uzuri katika kijana huyo alianza kumhubiri. Hapo mafundisho sahihi ya Islamu yalianza kuathiri moyoni.

Mian Muhammad Murad wakati wa kuenda Mkutanoni wa Mwaka wa 1924 alimchukua mwenyeji mmoja Bwana Allah Jawaya Msali, aliyerudi kwa athari nzuri sana kwa kuzuru Qadian na kuona mazingira ya pale. Lakini alipoulizwa na watu alianza kusema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu. Kwa Sodagar Mal hali hiyo ilikuwa swali kubwa. Aliona kwamba mkazi wa Qadian Mian Muhammad Murad anaishi maisha safi na matakatifu na watu wanasifu hulka zake lakini Allah Jawaya Msali anasema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu. Kusuluhisha tatizo hilo Bwana Sodagar Mal aliona muhimu kumwona Allah Jawaya peke yake. Basi Alimwita Allah Jawaya kwenye duka la ndugu zake wakikaa juu ya rundo la pamba alimwuliza kwamba unasema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu lakini huyo Muhammad Murad ni mbali sana na hali hiyo na anaishi maisha mazuri, kuna nini hapa?

Mara Allah Jawaya alisema kwamba kauli yangu ni uongo, mimi ni maskini wa kijiji, matajiri wa kijiji wanawapinga Waqadiani, kwa hiyo siwezi kusema kweli mbele ya watu. Nawaambia watu wa kawaida sawa na ridha yao ili wafurahi waila ukweli ni huu kwamba kama Islam inapatikana popote duniani basi ni katika Qadian tu. Nakuambia jambo hili la kweli, kama nikiwaambia watu wengine jambo hilo hilo, matajiri wa kijiji watanifukuza kutoka kijijini wakinipiga kwa viatu. Kwa hiyo mbele yao nitasema jambo lile lile. Lakini ukweli ni huu niliyokuambia. Kwa maongezi haya ya Allah Jawaya sio tatizo la Sodagar Mal liliondoka bali aliinuka humo kwa azma hii kwamba mimi mwenyewe nitaenda Qadian na nitashuhudia hali kwa macho yangu tu. Ingawa Sodagar Mal alichukia Islam kwa kuona hali duni, kutokuwa na elimu, kukosa hulka na hali mbaya ya kiuchumi ya Waislamu wa kawaida. Lakini mambo halisi ya kuvutia ya Mian Muhammad Murad na mfano wake mwema wa kushinda moyo alimlazimu kwamba akienda Qadian ashuhudie hali ilivyo mwenyewe. Wakati ule alibanwa na hali. Kwa ulimi alisema kwamba hata kama dunia yote isilimu sitasilimu lakini moyo ulivutika sana humo kwa nguvu.

Baada ya maongezi ya juu kwa Allah Jawaya kesho yake asubuhi tu Sadagar Mal akawa tayari kwenda Qadian. Alimwambia Mian Muhammad Murad kwamba ninaenda Qadian. Mian Muhammad Murad alisema kwamba maongezi yako ya jana usiku kwa Allah Jawaya niliyasikiliza kwa masikio yangu katika ngiza ya usiku. Wakati ule ule nilinuia moyoni kwamba kama Sodagar Mal akawa tayari kuenda Qadian basi nitaenda pamoja. Kwa hiyo naenda nawe.

Basi baada muda mfupi tu wote wawili waliondoka kwa kuelekea Qadian. Wakitoka Sangla Hill badala ya Batala walishuka Stesheni ya chini, stesheni mbele ya Batala, ili jamaa wa Sodagar Mal wakiwafuata isije wawakamate njia ya miguu kati ya Batala na Qadian. Msafara huo kutoka China ulifika Qadian. Sodagar Mal mara baada ya kufika Qadian alieleza katika nyumba ya wageni kwamba miye Mbaniani, kwa hiyo sitakula chakula kilichopikwa na Mwislamu yeyote. Siku zile mwalimu wetu Hadhrat Mir Muhammad Is'hak alikuwa msimamizi wa nyumba ya wageni na alipewa uwezo maalumu kutoka kwa Mungu ya kutumikia wageni. Basi alipanga kuagiza chakula cha Sodagar Mal kutoka nyumba ya Mabaniani na mpango huo uliendelea kwa wiki moja mfululizo. Katika muda huo Mian Muhammad Murad alimkutanisha Sadagar Mal na wazee wa Kiahmadiyya wapya waliosilimu kutoka Mabaniani na Masingasinga. Kukutana na ndugu Hadhrat Abdur Rahim ra, ndugu Hadhrat Abdur Rahman Qadiani, Hadhrat Masta Sardar Abdur Rahman B.A. ra Hadhrat Sheikh Ghulam Ahmad Waidh ra na Hadhrat Sheikh Muhammad Yusuf ra, Mhariri wa gazeti Nur Qadian kuliatharisha sana moyo wa Sadagar Mal, kwani watu hao walitokana na Masingasinga na Mabaniani. Na kwa kusilimu walipata nuru maalumu na maisha ya kiroho. Mian Muhammad Murad alimkutanisha na wazee Waislamu wa zamani pia ambao walipata Baraka maalumu za Jumuiya Ahmadiyya. Maongezi yaliyojaa na ikhlasi na mifano bora ya Hadhrat Maulawii Rajiki ra, Mualimu wangu Hadhrat Hafidh Roshan Ali ra, Hadhrat Khalifa Rashiduddin ra, Hadhrat Maulawii Dhulfikar Ali Khan ra na Hadhrat Maulawii Abdul Mughni ra ililazimu moyo wa Sodagar Mal kuwa Sheikh Abdul Qadir.

Bado ikawa wiki moja tu tangu Sodagar Mal aje Qadian, kundi la watu saba cha jamaa yake wakaja Qadian kwa kumrudisha. Watu hao walimwona Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan, siku zile aliyekuwa Nadhir Aalaa kiheshima na walisisitiza kwamba Sodagar Mal arudishwe nao. Bwana Chaudhari alisema kwamba ni mafundisho ya Islam:

لا اکراہ فی الدین

kwamba *hakuna karaha katika dini* wala hiyo haijuzu. Kama Sodagar Mal akitaka kuenda nanyiasi bila shaka mchukueni.

Jamaa walimwambia Sodagar Mal kuenda nao kwao lakini yeye ameshakuwa Abdul Qadir moyoni. Kwa hiyo alikataa kwenda nao na alianza kuishi katika makao ya kutangaza Islam katika hali yoyote.

Siku ya pili au tatu Sodagar Mal alimwomba Khalifatul Masihi II akikubali baiti yake amwingize katika Jumuiya Ahmadiyya. Hapo Hudhur ra alisema kwamba kuna haraka gani. Subiri miezi 2-3 zaidi lakini aliomba kwa usisitizo kwamba Hudhur, nimeshapata yakini juu ya ukweli wa Islam. Hapo Hudhur ra alimwambia mwalimu wangu Hadhrat maulana Seyyid Muhammad Sarwar Shah ra kwamba msomeshe shahada leo leo, kesho tutapokea baiati. Basi itafanyika hivyo, sasa Lala Sodagar Mal akawa Sheikh Abdul Kadir. Alhamdulillah, thumma Alhamdulillah.

Ilikuwa athari kubwa ya tamaduni ya kibaniani kiasi hiki kwamba juu ya kusilimu mwanzo mwanzoni Bwana Sheikh alikuwa akila chakula kwa shida sana kilichopikwa na Mwislamu. Lakini baada ya siku chache aliungana kiasi hiki kwamba ikawa ngumu kutambua kwamba kijana huyu amesilimu kutoka kwa mabaniani au ni Mwislamu wa kuzaliwa. Kwa kweli mabadiliko hayo kikamilifu yalikuwa matokea ya lazima ya ikhlasi ile aliyokuwa na Sodagar Mal moyoni mwake kwa dini. Islam ilinurisha sana ikhlasi hiyo.

Ilipopita miezi michache tu tangu Sheikh Abdul Qadir alipata kuzaliwa kiroho, Pandat Mashuhuri wa Sanatan Dharm Bwana Raj Narain Arman akaja Qadian. Sheikh Abdul Qadir alishajiunga na Madarasa Ahmadiyya. Mabaniani wachache wa Qadian walimleta Pandat Raj Narain kwa kumtembeza Madarasa Ahmadiyya. Kwani Kutoka Madarasa Ahmadiyya tu wabashiri vijana walikuwa wanatoka ambao walishindana na Aariya Samaj na Ukristo kwa ujasiri sana. Kwa bahati tu wakatu ule Sheikh Abdul Qadir, Mwislamu Mpya alisimama uani na Mabaniani wa Qadian walishajua kusilimu kwake. Mbaniani mmoja akimwashiria Bwana Sheikh alimwambia Bwana Pandit Kwamba kijana huyu pia alikuwa mbaniani lakini sasa ameshasilimu. Bwana Pandit alimwendea Sheikh Abdul Qadir moja kwa moja na kamwuliza kwamba Islamu ina uzuri gani ambao unakosekana katika dini ya Kibaniani. Baada ya kutafakari kidogo kijana Abdul Qadir alimwuliza Bwana Pandit kwamba uniambie kwamba lengo la dini ni nini? Bwana Pandit alijibu kwamba kukutana na Mungu. Hapo Abdul Qadir alisema kwamba umeshapata kukutana na Mungu? Bwana Pandit alijibu kwamba hapana. Hapo Bwana Sheikh alimwuliza kwamba sawa na elimu yako je, kuna Mbaniani mzima aliye mkutana na Mungu? Sasa pia Bwana Pandit alikanusha lakini pamoja alisema kwamba naweza kusema kuhusu Bwana Ram Chandar na Bwana Karishna. Sheikh Abdul Qadir alsema kwamba nataka kumwona Mbaniani yeyote wa namna hii katika zama hizi. Hapo Bwana Pandit alimwuliza kijana Mwislamu Mpya kwamba je, waweza kutaja jina la Mwislamu yeyote ambaye amepata kukutana na Mungu. Bwana Sheikh mara alitaja jina la Hadhrat Masihi Mau'udi as na alieleza kama ukweli wake ufunuo:

یاتون من کل فج عمیق

yaani *watu watamfikia kutoka sehemu mbali mbali*. Hapo Mabaniani waliokuwa pamoja walimwita Bwana Pandit na walienda upande mwingine.

Maongezi hayo ya kawaida ambayo Sheikh Abdul Qadir aliyofanya katika siku zake za awali na mjadili mkubwa wa Kibaniani yanaonyesha wazi wazi jambo hili kwamba Bwana Sheikh alikuwa makini kwa itikadi yake na kijana mwekaje lengo lake mbele yake.

Sasa Bwana Sheikh alikuwa miongoni mwa wanafunzi wazuri wa Madarasa Ahmadiyya, mwanafunzi mwenye heshima na juhudi. Katika 1931 alipata shahada ya usheikh katika mtihani wa chuo cha Panjab (Panjab University). Baada ya kupata mazoezi ya mahubiri kwa muda fulani katika 1934 alianza kazi ya mahubiri.

Bwana Sheikh alikuwa akitoa hotuba yenye athari lakini alikuwa akiepa tu kutoa hotuba iwezekanavyo sawa na tabia yake. Alikuwa akiongea kwa jazba na sauti ya athari katika mjadala. Alikuwa akimkamata vizuri mpinzani.

Baada ya uhuru wa Pakistan, alihamia pale na aliendelea kutumukia dini ya Mungu.

# Maarifa Juu ya Jahanamu na Peponi

*Kutoka uk. 4*

kuwa ni ya kinuru na mingine ya kigiza inayotengenezeka kutokana na mwanga au giza la matendo. Ingawaje siri hii ni nyepesi, lakini inaeleweka akilini. Binadamu mkamilifu huweza kupata katika maisha haya haya mwili mmoja wa nuru zaidi ya mwili wa kiwiliwili, na ipo mifano yake mingi inayoonekana katika hali ya kashfi. Ijapokuwa ni vigumu kumfahamisha habari hii mtu mwenye akili ya kawaida, lakini wale wanaowahi kupata kashfi kiasi fulani hawatastaajabu juu ya mwili huo unaoumbika kutokana na vitendo, bali watasikia ladha katika maelezo haya.

Kisha baada ya Barzakh kuna zama ziitwazo Ufufuo. Katika zama hizo kila roho, njema au mbaya, nzuri au asi, itajipatia mwili mmoja wa kuonekana hasa; siku hiyo imewekwa kwa Onyesho kamili la Mungu ambapo kila mtu atatambua dhati ya Mola wake barabara, na kila mmoja atafikia upeo wa mwisho katika malipo yake. Msistaajabu kwamba Mungu atawezaje kufanya hivyo, kwani Mungu anao uwezo wote na hufanya apendavyo jinsi Anavyosema Mwenyewe:

Je, mwanadamu hatambui ya kwamba Tumemwumba kwa tone la manii lililotiwa katika tumbo la uzazi? Lakini lo! amekuwa hasimu dhahiri. Akatupigia mfano na kusahau umbo lake, akaseme: Nani ataihuisha mifupa na hali imesagika? Waambie, Ataihuisha Aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila namna ya kuumba (36:78-80). Shani ya amri yake ni kwamba anapokusudia kipatikane kitu fulani anasema tu kuwa, basi huwa. Basi ni Mtukufu ambaye anao ufalme juu ya kila kitu, nanyi nyote mtarejeshwa Kwake. Katika aya hizi, Mwenyezi Mungu Ameeleza kwamba hakuna kisichowezekana kwake. Yule aliyeumba binadamu kutokana na tone dhaifu, je atashindwa kuumba mara ya pili?

Sawa na Kitabu cha Mungu malipo ya mwema na mbaya yatatolewa katika mahali pawili. Kwanza katika Barzakh ambako kila mmoja atapata malipo yake kisirisiri. Waovu wataingia motoni mara baada ya kufa na wema watastarehe Peponi mara wafapo. Ziko aya nyingi ndani ya Kurani Tukufu zinazosema kwamba mtu mara akifa huanza kuona malipo ya matendo yake. Kuhusu mja mmoja aendaye Peponi Mungu Anasema: Akaambiwa: Ingia Peponi Surah 36:27. Kadhalika kuhusu aendaye Motoni anasema Surah 37:56;

Mja mmoja alikuwa na rafiki mbaya; wote walipofariki, yule mja wa Mungu akasema yu wapi rafiki yangu? Mara akaonyeshwa yuko katikati ya Jahanamu. Kwa kifupi, thawabu na adhabu huanza mara baada ya kufa: waendao Motoni huingia Motoni na wenye Pepo huingia Peponi. Lakini baada yake, kuna siku nyingine ya Dhihirisho Kuu la Mungu aliyoweka Mwenyezi Mungu kwa hekima Yake kubwa. Kwani Yeye aliumba binadamu ili Atambulikane kuwa Mwumba. Kisha atawaangamiza wote ili Ajulikane kuwa Kahari. Kishapo Akiwapa wote uhai kamili Atawakusanya uwanjani ili Atambuliwe kwa njia ya uwezo wake. Hilo nililoeleza ni jambo la pili la maarifa kuhusu akhera.

Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu uk 133 - 141

Katika maisha haya Duniani tumepewa dalili mbalimbali juu ya Akhera, Kisha tumeona/ sikia wenzetu wakipatwa na athari za matendo mema na ubaya. Ila tumeshuhudia juu matokeo mema ya matendo mema na adhabu pia. Majanga ya asili ni sehemu ya athari ya matendo yetu.

Pia tumeshuhudia namna Matendo yetu yanavyo weza kuumbika katika Njozi na Usingizini Mfano wa Kifo na Usingizi ni Kifo Surah 39:43. Kama katika Usingizi ambao ni Kifo cha muda usiku Matendo yanaumbika katika Njozi na ndivyo katika Kifo cha moja kwa moja Matendo yetu yatakavyo jipatia umbo sawa na matendo yetu.

Katika matoleo yajayo tutaangalia Maarifa ya Tatu juu ya Jahanamu na Peponi, Insha Allah.

Mola wetu, tumiminie uvumilivu na Utufishe watii. Amin

# Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

*Kutoka uk.12*

Hadhrat Umar ra akamwambia usiende mbele. Utosheke na haya uliyoyafanya. Wewe badala yake nenda ukaimarishe mambo ya utawala ya miji iliyotekwa.

Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra ndiye aliyestawisha mji wa Kufa na akayakalisha makabila ya Waarabu katika sehemu zake mbalimbali. Watu wa Kufa wakalalamika mbele ya hadhrat Umar ra kuhusiana na hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas kuwa yeye si kiongozi mzuri kwa sababu yeye hajui hata kusalisha sala. Hadhrat Umar ra akamwita na kumweleza kuwa haya ni malalamiko dhidi yako. Yeye akajibu mimi nasalisha sala ile aliyosalisha mtume saw. Yaani rakaa mbili za mwanzo ninarefusha na rakaa mbili za mwisho ninazifupisha. Hadhrat Umar ra akajibu mimi nilikuwa ninatarajia haya haya kutoka kwako. Hadhrat Umar ra akamtuma mtu mmoja akiambatana na hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra kwenda kuchunguza uhakika wa mambo hayo. Wakaenda katika kila msikiti wa Kufa na kuuliza kuhusu utendaji wa hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a. Watu wa misikiti yote wakajibu tunamwona kuwa ni kiongozi mzuri isipokuwa katika msikiti mmoja. Mtu mmoja akadai kuwa hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a. alikuwa haendi vitani pamoja na jeshi wala alikuwa hagawi mali sawasawa. Ndipo hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a. alipoomba dua kuwa kama mtu huyu ni mwongo basi Mwenyezi Mungu arefushe sana maisha yake akiwa omba omba. Ndipo alipozeeka sana na kudhoofika sana kwa sababu ya uzee mpevu. Akawa anasema hali yangu hii ni kwa sababu ya dua ya hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra. Kwa sababu mimi nilisema uongo juu yake.

Hadhrat Umar ra katika siku zake za mwisho karibu na kufariki kwake aliunda kamati itakayomchagua Khalifa, ndani ya wajumbe wake alikuwepo hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra. na akaagiza kuwa kama hadhart Sa'ad bin Abi Waqas atachaguliwa kuwa Khalifa itakuwa vizuri zaidi, lakini kama mtu mwingine atachaguliwa Khalifa basi hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas awe mshauri wake.

Hadhrat Athuman alipochaguliwa kuwa Khalifa alimfanya hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas kuwa Gavana wa Kufa lakini baadae alimwita kurudi Madina.

Na hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas akaachana na mambo yote ya utawala na akakaa pembeni.

Hadhrat Muslih Maud ra akiwasafisha masahaba kutokana na fitna iliyotokea katika zama za Ukhalifa wa hadhart Uthman ra anasema ili kuondoa fitna hii masahaba walikuwa katika makundi mawili. Moja ni la wale masahaba wakubwa wenye uzoefu na la pili ni la vijana wapya. Kundi la kwanza lilijitahidi kuwaelewesha watu wengine umuhimu wa ukhalifa na hasara ya fitna, na kundi la pili la vijana walikuwa na jukumu la kumlinda hadhrat Uthman ra. Katika kundi la kwanza walikuwemo hadhrat Ali ra na hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas na vilevile masahaba wengine wakubwa. Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas alifanya jitihada kubwa kuondoa fitna hii ingawaje hali yake ya kujitenga hakuiacha wakati wa hadhrat Uthman na hata wakati wa hadhrat Ali ra.

Hadhrat Amir Muawiya alimwita hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra akimshawishi aungane na jeshi lake ili kupigana dhidi ya upande wa ukhalifa. Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra akamjibu kwamba: Hadhrat Ali alikwisha niita kabla yako na yeye ni bora zaidi kuliko wewe lakini mimi sikuenda kuungana naye. Kama mimi nimemkatalia yeye itawezekanaje mimi kujiunga na wewe ili kupigana dhidi yake Ali ra kwani siku moja ya Ali ra ni bora kuliko miaka yako elfu moja. Nami siwezi kushiriki katika vita yoyote kwa sababu jambia langu haliwezi kutofautisha kati ya muislamu na kafiri. Akimaanisha kuwa panga langu lilitumika wakati wa mtume saw kupigana na kuua makafiri lakini kama sasa hivi nitapigana panga langu litaua waislamu. Jambo ambalo si zuri hata kidogo, ndio maana katika siku zile za fitna yeye alikaa kando.

Mtu mmoja alimwuliza kwa nini una mahusiano mazuri na Maanswar. Yeye akajibu mtume saw amesema mtu yule aliye mwaminio halisi atakuwa na mahusianao mazuri na Maanswar na yule ambaye ni mnafiki atakuwa na uadui nao.

Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas alifariki katika mwaka wa 55 Hijria. Baadhi ya watu wana maoni kuwa alikuwa na umri wa miaka zaidi ya sabini wengine 74 na wengine 81. Katika mwaka wa kufariki kwake pia kuna hitilafu. Yeye alifariki katika eneo lililo mbali kidogo na mji wa Madina. Watu kwa mapenzi yao walilibeba jeneza lake kutoka sehemu ile mpaka Madina. Sala ya jeneza lake ilifanyika katika msikiti wa mtume saw na wake wa mtume saw pia walishiriki katika sala ya jeneza lake na Marwan bin Hakam aliongoza sala ile. Yeye katika Muhajirina alikuwa ni mtu wa mwisho kufariki.

Na maiti yake iliwekwa kwenye kanzu aliyovaa alipopigana vita vya Badri kama sanda sawa na alivyousia. Wale masahaba waliopigana vita vya Badri walikuwa wanaheshima zaidi kuliko masahaba wengine na wale walioshiriki katika vita hii wao wenyewe walikuwa wanaona fakhari kwa sababu yake.

Baada ya kumaliza hotuba hii hadhrat Khalifatul Masihi V atba alitaja wanajumuiya waliofariki. Akataja sifa zao na huduma zao walizozifanya kwa jamati na akawaombea Mwenyezi Mungu apandishe daraja zao katika ubora.

Wanajumuiya hawa ni bwana Safdar Ali, bi Iffat Nasiir, bwana Abdulrahim Saqi na bwana Said Ahmad. Khalifa mtukufu atba alisema nitaongoza sala ya jeneza zao baada ya sala ya Ijumaa.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

Dh. Qd - Dh. Hj 1440 AH | AGOSTI 2020 | ZAHOOR 1399 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu**saw

Imesimuliwa na hadhrat Ibn Umarra ya kuwa: Mtumesaw alisema: "Msijihusishe katika mazungumzo mengi isipokuwa yanayohusika na kumkumbuka Allah. Maana kuzungumza sana bila ya kumtaja Allah huufanya moyo kuwa mgumu! Na mtu aliye mbali sana na Allah ni mwenye moyo mgumu" (**Tirmidh**)

# Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 14/08/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmadatba (**'A**yyadahullahu **T**a'ala **B**i-Nasrihil **A**ziiz') alisema;

Wiki mbili zilizopita mazungumzo kumhusu hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a yalikuwa yanaendelea. Leo pia tutaendeleza mazungumzo yale.

Katika vita moja alikuwepo Muislamu mmoja mhalifu aliyekuwa amefungwa minyororo kwa sababu ya adhabu. Yeye alikuwa ana mapenzi makubwa ya kushiriki katika vita vya Jihadi. Akamwambia mjakazi mmoja wa hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a kuwa naomba unifungue nikashiriki vita. Nikirejea unaweza kunirudisha kunifunga katika minyororo. Adhabu hii ilitokana na yeye kunywa pombe. Hadhrat Sa'ad akamwona vitani akipigana kwa umahiri mkubwa. Vita ilipokwisha akarudi kwenye minyororo. Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a akamwacha huru kwa sharti kuwa kama akinywa tena pombe atamuadhibu tena.



*Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih Vatba huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.*

Khalifa mtukufu atba anasema kisa hiki, hadhrat Muslih Maud ra amekisimulia katika aina yake. Mhalifu yule Muislamu alikuwa ni kiongozi wa kabila fulani la Waarabu, lakini yeye hakuweza kuacha tabia ya kunywa pombe. Kwa hiyo adhabu yake ikawa kufungwa katika minyororo. Maaskari waliporudi kutoka vitani wakawa wanazungumza kwamba Waislamu wamepata hasara kubwa sana vitani. Yeye akawambia kama mimi nikipata nafasi ya kwenda kupigana nitawaonesha umahiri na ujasiri wangu. Mke wa hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a akasikia. Yule mfungwa akasema uniachie huru nikapigane vita nikirudi unifunge tena katika minyororo. Yeye akaenda vitani akapigana kwa umahiri mkubwa kiasi kwamba Waislamu wakaanza kupata ushindi na kusonga mbele.

Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas r.a alipomwona vitani akasema nikijua mtu aliyemwaachia mtu huyu huru nitamwadhibu. Mkewe akasikia, ndipo aliposema kwa hasira nimemwacha mimi huru. Wewe ulikuwa umekaa bure tu kwenye kibanda ukiangalia na kuwaamrisha wengine. Na huyu alikuwa mstari wa mbele katika uwanja wa vita akipigana kwa umahiri mkubwa. Kisa hiki hadhrat Muslih Maud ra amekisimulia akikihusisha na huduma ya wanawake kwa dini ya Kiislam.

Kuna kisa kingine alichokitoa kuhusiana na huduma ya akinamama kwa dini ya kiislam. Katika vita vya Qadsia watoto wanne wa mama mmoja aitwaye hadhrat Khansaa ra walishiriki. Walipigana kwa uhodari mkubwa. Mwishowe wote wanne waliuawa, lakini mama huyu hakulia wala kuhuzunika. Badala yake alitangaza kwa fakhari kubwa kuwa namshukuru Mwenyezi Mungu kwani watoto wangu wote wanne wamepata ushahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Baada ya ushindi wa vita vya Qadsia na Madain hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas ra akamwomba hadhrat Umar ra rukhsa ya kusonga mbele.

*Endelea uk 11*

KITABU KIPYA




*Na*

Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad

*Khalifatul Masihi wa pilira*

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LIMITED

## Muhisani wa Ubinadamu

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa hotuba tatu zilizotolewa na Hadhrat Mirza bashiruddin Mahmood Ahmad r.a. Khalifa wa pili wa Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Duniani katika mada ya historia ya maisha yaliyobarikiwa na sifa za Mtukufu wa Islam (Rehema na Amani ziwe juu yake).

Ya kwanza ya hizi hotuba ilitolewa mnamo mwaka 1928 na nyingine mbili mnamo 1933 katika kuadhimisha sifa tukufu za Mtume Mtukufu wa Islam (Rehema na Amani ziwe juu yake). Huu ulikuwa wakati ambao wapinzani wa Islam walianzisha kampeni potofu za kukashifu na kuichafua taswira ya Mtukufu Mtume wa Islam (Rehema na Amani ziwe juu yake) barani Hindi kote.

Ni katika pazia hili la kihistoria ambapo mwandishi huyu adhimu anatoa hoja kwamba Mtukufu Mtume wa Islam (Rehema na Amani ziwe juu yake) hakuwa tu Mhisani mkubwa kabisa wa ubinadamu bali pia ni Mbora wa Mitume, ambaye athari yake tukufu itaendelea kuzisafisha nyoyo hadi siku ya mwisho.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 3300/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com